SHULE YA SEKONDARI KITWANA,
S.L.P 110.
KAHAMA.
Barua pepe: *kitwanasec@gmail.com*
Mob: 0759 499 090/ 0683 731 220
Tarehe: ......................

Kumb.Na.KSS/J/01/VOL.1/03
Jina la mwanafunzi ______________________________
S.L.P __________________________
______________________________

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KITWANA HALMASHAURI YA MJI WA KAHAMA, MKOA WA SHINYANGA**

## 1.0. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha ________ katika Shule ya Sekondari Kitwana mwaka ________. Shule hii ipo umbali wa Km 10 kutoka Stendi Kuu ya Mabasi Kahama.

Usafiri wa kutoka mjini Bajaji/ Pikipiki unapatikana vituo vya mjini Kahama, nauli ni Tshs.5000/= kwa bajaji na Tshs.3,000/= kwa pikipiki.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe ____________ unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe _____________. Unatakiwa kuwa umeripoti shuleni ndani ya siku saba.

## 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

**WAVULANA**

i) Suruali mbili mpya rangi nyeusi, mashono zisiwe pana sana, marinda mawili. Suruali za kubana (modo) na mitindo ya aina yoyote haziruhusiwi. Kipande cha sare kimeambatanishwa kwenye hii fomu ya kujiunga.
ii) Mashati meupe mawili mapya mikono mifupi kitambaa cha tetroni
iii) T-shirt rangi ya Brown na sweta rangi ya kijivu (zinapatikana shuleni)
iv) Soksi nyeusi jozi mbili, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visigino vifupi visivyochongoka.
v) Sare za michezo, kaptula ya kaki na raba rangi yoyote
vi) Wavulana hawaruhusiwi kufuga kucha, kufuga nywele ndefu, kupaka rangi kwenye kucha na kuweka dawa kwenye nywele.

**WASICHANA**

i) Sketi mbili mpya rangi nyeusi, mashono urefu iguse kisigino chini, marinda makubwa, kiuno (waist) 1½ isiwe na mikanda. Kipande cha sare kimeambatanishwa kwenye hii fomu ya kujiunga.
ii) Mashati meupe mawili mapya mikono mifupi kitambaa cha tetroni kisichoonyesha nguo za ndani
iii) T- shirt rangi ya Brown na sweta rangi ya kijivu (zinapatikana shuleni)
iv) Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visigino vifupi visivyochongoka na soksi nyeupe jozi mbili
v) Sare za michezo sketi ya kaki na raba rangi yoyote
vi) Wasichana hawaruhusiwi kusuka, kuweka dawa nywele, kufuga nywele ndefu, kufuga kucha au kupaka rangi kwenye kucha.
vii) Kwa waislamu, rangi ya Hijab ifanane na sare za shule

**NB:** Kwa wanafunzi wote, wavulana na wasichana mavazi ambayo hayaendani na maagizo, yaliyotolewa hapo juu yatapelekea kusimamishwa masomo mara moja

2.2 MZAZI /MLEZI UNATAKIWA KUMNUNULIA MWANAO MAHITAJI YAFUATAYO:-

i) Madaftari makubwa 12 (Counter book quire3)
ii) Kalamu za wino
iii) Penseli na kifutio
iv) Mathematical set
v) File moja la plastiki kwa ajili ya kuhifadhia taarifa/ kumbukumbu za wanafunzi
vi) Begi la shule **(mifuko ya nguo na plastiki hairuhusiwi)**
vii) Slasher (fyekeo) kwa ajili ya usafi (Wasichana)
viii) Jembe kwa ajili ya usafi (Wavulana)
ix) Mfagio mmoja wa chelea wenye mpini

2.3 KADI YA BIMA

Mwanafunzi aje na kitambulisho cha BIMA ya afya ya CHF/NHIF, na kwa wale ambao hawana kadi, TAFADHALI MZAZI/MLEZI UJE NA TSHS.5,000/= UNAPOMLETA MWANAO SHULENI NA ATAPATIWA BIMA YA CHF SIKU HIYO NA WATAALAM WA AFYA

3.0 KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

3.1 Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule;

i) Wizi
ii) Uasherati
iii) Ubakaji
iv) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
v) Kupigana au kupiga
vi) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii) Kudharau Bendera ya Taifa
viii) Kuwa mjamzito/ kupata mimba
ix) Kutoa mimba
x) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au wa watu.
xi) Kukataa adhabu kwa makusudi
xii) Kuwa na simu ya mkononi

3.2 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule

4.0 Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KITWANA SEKONDARI**

.............................

BASIL KIJAZI KIHIYO
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI KITWANA
S.L.P. 110 KAHAMA

| PICHA /STAMP SIZE YA MWANAFUNZI | | PICHA /STAMP SIZE YA MZAZI |
|---|---|---|

# SHULE YA SEKONDARI KITWANA

## FOMU YA KUKUBALI MASHARTI YA SHULE

1. Mimi (Jina la Mwanafunzi) ............................................... kidato cha ......... naahidi kutii na kutekeleza masharti na maelekezo mbalimbali ya shule hii na uongozi wa shule kwa ujumla. Kama mwanafunzi, naahidi kuwa mtii na mnyenyekevu mahali pote pamoja na kuzitii kanuni zote za shule.

2. Nikikiuka sheria, kanuni na taratibu za shule niadhibiwe ninavyostahili, hata kufukuzwa shule.

3. Mimi mzazi/ mlezi nakubaliana na masharti yote ya shule, nitatekeleza masharti na maagizo yote ya shule.

4. ..................................................... ..........................................

   **Jina la Mwanafunzi** **Jina la mzazi/ mlezi**

5. ..................................................... ..........................................

   **Sahihi ya Mwanafunzi** **Sahihi ya mzazi / mlezi**

**Tarehe:** ...................................

Anwani kamili ya Mzazi/ mlezi/ mtaa unaoishi

.......................................................

.......................................................

.......................................................

Na. ya simu ya Mkononi

.......................................................

.......................................................

.......................................................

**NB:** Fomu hii inatakiwa kuletwa shuleni siku mwanafunzi anaporipoti

# MAELEZO BINAFSI (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI)

1. Jina kamili la mwanafunzi;..........................................................

2. Tarehe ya kuzaliwa;..................................................................

3. Jina la baba/mlezi;..................................................................

4. Kazi afanyayo baba /mlezi;..........................................................

5. Jina la mama/mlezi;..................................................................

6. Kazi afanyayo mama /mlezi;..........................................................

7. Anwani ya baba/mama;................................................................

8. Ana kilema chochote;.................................................................

9. Anapendelea kushiriki michezo gani;.............................................

10.Ndugu wa mwanafunzi

Taja ndugu wasiopungua watano wa karibu wanaoweza kutoa msaada kwa mwanao;

| s/na | JINA | UHUSIANO | KAZI | SIMU/ANWANI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |

THE PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
MEDICAL EXAMINATION FORM

From:
THE HEADMASTER,
KITWANA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 110,
**KAHAMA.**

To,
The Medical officer,
Government Hospital,
P.O.BOX 472,
Kahama.

Please examine the student called ................................................... and indicate if he/she is fit/not fit to join /continue with studies.

1. Blood test ..............................................
2. Chest ..............................................
3. Asthma ..............................................
4. TB – Test ..............................................
5. Typhoid ..............................................
6. Pregnancy for female ..............................................
7. Operation ..............................................
8. Epilepsy ..............................................
9. Vision ..............................................
10. Hearing ..............................................
11. Skin disorder ..............................................
12. Others (please specify) ..............................................

..............................................

..............................................

**DOCTOR'S DECLARATION**

I have examined the above mentioned student, he/she/is fit/not fit for schooling.

Signature ......................... Title ............................. Date: ................

STAMP OF MEDICAL OFFICER